

MAAFISA MALIASILI WAPANDISHWA KIZIMBANI KWA UHUJUMU UCHUMI

Na Mussa Misalaba, Dar Es Salaam

Watu watatu wakiwemo maafisa wawili wa wizara ya Maliasili na Utalii na mwindaji wa wanyamapori, wamepandishwa kizimbani kwenye mahakamani ya Hakimu Mkazi Kisutu Alhamisi iliyopita kwa mashtaka sita ya rushwa likiwemo la kuisababishia hasara serikali.

Washtakiwa hao ni afisa wanyamapori anayehusika na matumizi endelevu ya wanyamapori, Mohamed Madehele(55); afisa wanyamapori anayehusika na ukusanyaji wa mapato ya uwindaji wa wanyamapori, Rajab Hochi (41); na mwindaji wanyamapori wa Northern Hunting Enterprises company Limited, Isaac Maji (47).

Mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Wilbard Mashauri, waendesha mashtaka wa TAKUKURU, Leonard Swai na Pendo Temu, katika shtaka la kwanza hadi la tano, walidai kuwa kati ya Oktoba 12, 2008 na Desemba 31, 2011 Hochi na Madehele walitenda makosa ya matumizi mabaya ya madaraka yao ya ajira.

Waendesha mashtaka waliambia mahakama kuwa katika kipindi hicho washtakiwa kwa makusudi walishindwa kukusanya faini toka Northern Hunting Enterprises Company Limited takribani Dola za Marekani 32,599.14 kutokana na kuzidisha idadi ya wanyama walioruhusiwa kuwinda.

Kitendo cha washtakiwa kushindwa kwa makusudi kukusanya faini za uzidishaji wanyamapori waliowindwa kiliinufaisha isivyohalali kampuni ya uwindaji wanyamapori ya Northern Hunting Enterprises Company Limited kiasi cha Dola za Marekani 32,599.14 kinyume na kanuni za fedha za umma za mwaka 2001.

Katika shtaka la sita, Upane wa mashtaka ulidai kuwa kati ya Oktoba 12, 2008 na Desemba 31, 2011 washtakiwa wote watatu kwa pamoja na ujumla wao na kwa makusudi waliisababishia hasara Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dola za Marekani 32,599.14 kutokana na faini kutokusanywa.

Washtakiwa wamekana mashtaka na upande wa mashtaka uliambia mahakama kuwa uko tayari kwa ajili ya kusikiliza hoja za awali kwa kuwa uchunguzi wa shauri umekamilika na haukuwa na pingamizi dhidi ya dhamana za washtakiwa kwa masharti ambayo yangetolewa na mahakama.

Masharti ya dhamana waliyopewa washtakiwa na mahakama ni kuwa na wadhamini wawili kila mmoja ambao walitakiwa kusaini bondi ya Shilingi milioni 50 pamoja na mmoja wao kuwa na hati ya mali isiyohamishika isiyopungua Shilingi milioni 50.

Masharti mengine ni mmoja wa wadhamini kuwa na barua ya utambulisho toka serikali ya mtaa na washtakiwa hawaruhusiwi kutoka kutoka nje ya mkoa wa Dar es Salaam bila kibali cha mahakama.

Hochi alitimiza masharti ya dhamana hivyo aliachiwa huru huku Madehele na mwenzake Maji, aliyekuwa akitetewa na wakili wa kujitegemea Benjamin Mtwanga, wakipelekwa mahabusu hadi Januari 31mwaka huu kesi itakapokuja kwa ajili ya kutajwa.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka matano ya matumizi mabaya ya madaraka kinyume na kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Washtakiwa wanadaiwa kutenda kosa la kuisababishia hasara serikali, kinyume na aya ya 10(1) ya Jedwali la Kwanza na vifungu namba 57(1) na 60(2) vya sheria ya uhujumu uchumi sura ya 200 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.